## 5.2 KISWAHILI (102)

MANYAM FRANCHISE
Discover!Learn!Apply

### 5.2.1 Kiswahili Paper 1 (102/1)

1. Hii ni kumbukumbu. Mtahiniwa azingatie vipengele viwili vya kimsingi vya utungo wa aina hii; yaani muundo/ sura na yaliyomo/ maudhui.

(a) **Sura ya kumbukumbu/ muundo wa kumbukumbu**

1. Kichwa kikuu - kichwa hiki kijumuishe:
   - jina la mkutano/ kundi linalokutana
   - mahali pa mkutano
   - siku ya mkutano
   - tarehe ya mkutano
   - saa

2. Mahudhurio
   (a) Waliohudhuria
   (b) Waliotuma udhuru
   (c) Waliokosa kuhudhuria
   (d) Waalikwa/ waliokuwepo ila si wanabaraza kwa mfano, mkuu wa ushauri nasaha (Hii si lazima, ila yaweza kutuzwa kama upekee wa mtahiniwa)
3. Ajenda
4. Kufunguliwa kwa mkutano
5. Kumbukumbu zenyewe ziandikwe kwa utaratibu mwafaka
6. Kimalizio

(b) **Mwili/ Maudhui**
Yaliyomo yashughulikiwe hapa:
Mtahiniwa ajibu swali alililoulizwa kwa kujadili suala la ukiukaji wa sheria za shule na kupendekeza namna ya kuukomesha.

Baadhi ya hoja za kuzingatia:

(i) **Visa vya ukiukaji wa sheria**
- matumizi mabaya ya dawa
- matumizi mabaya ya mtandao wa intaneti
- mahusiano yasiyofaa, kwa mfano, usagaji na ubasha
- matumizi ya simu tamba(rununu)
- kutoroka shule
- kutowaheshimu wakuu
- baadhi kutozingatia usafi wa mwili na mazingira
- kuzorota kwa utenda kazi darasani. Kwa mfano baadhi kutofanya mazoezi/ kazi wanayopewa na walimu
- udanganyifu katika mtihani na majaribio endelevu
- kuwanyanyasa wanafunzi wenzao
- kujitenga katika makundi ya kijamii na kiuchumi

(i) **Sababu za kukiuka sheria**
- ukosefu wa mawasiliano kati ya wanafunzi na usimamizi wa shule



Powered By: www.manyamfranchise.com

- sheria zisizowapa wanafunzi uhuru/ sheria kandamizi
- uongozi dhalimu
- ukosefu wa uwajibikaji wa uongozi
- athari za dawa za kulevya
- shinikizo la marika
- matatizo ya wanafunzi kutoshughulikiwa/ wanafunzi kuhisi hawashughulikiwi
- vielelezo vibaya kutoka kwa wanajamii kuhusu usuluhishaji wa migogoro.

(ii) **Namna ya kukomesha hali hii**

- wanabaraza kuwa kiungo kati ya wanafunzi na uongozi wa shule
- kuimarishwa kwa mawasiliano kati ya wanafunzi na walimu/ uongozi wa shule
- kuimarishwa kwa ushauri marika
- uongozi kumjali mwanafunzi
- wanabaraza kufanya mikutano mara kwa mara na wanafunzi ili kuwaelezea sera za shule
- baraza kushiriki katika vita dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya
- sheria za shule kuchunguzwa upya mara kwa mara ili kubadilisha vipengele ambavyo huenda vikahisika kumnyanyasa mwanafunzi
- kuwahusisha wanafunzi katika kutoa mapendekezo kuhusu utatuzi wa matatizo yao.

**Tanbihi**

I Sehemu nne kuu za kumbukumbu zijitokeze kama ifuatavyo:

(a) **Kichwa/ anwani**

(b) **Mahudhura/ mahudhurio**
Yaanze kwa walio na cheo, kama vile Mwenyekiti wa Baraza, Katibu wa Baraza

(c) **Ajenda**
Ziorodheshwe kwa kufuata kielekezi kifuatacho:

1. Kufunguliwa kwa mkutano/ wasilisho la mwenyekiti
2. Kupitia kumbukumbu za mkutano uliotangulia/ kusomwa na kuidhinishwa kwa kumbukumbu za mkutano uliotangulia
3. Yaliyoibuka/ yaliyotokana na kumbukumbu hizo (baadhi ya hoja zinaweza kujadiliwa hapa). Ubunifu wa mtahiniwa unaweza kuanza kukadiriwa hapa
4. Ripoti kuhusu shughuli za mwezi (hoja nyingine zijadiliwe pia/ visa vya ukiukaji wa sheria za shule)
5. Visa vya ukiukaji wa sheria za shule
6. Mchango wa Baraza katika kukabiliana na visa hivi
7. Masuala mengineyo/ shughuli nyinginezo
(mtahiniwa ataibuka na ajenda yake, mradi ihusiane na swali)

(d) **Kumbukumbu zenyewe**
Matukio yaandikwe kwa utaratibu wa nambari.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Kila hoja inayojadiliwa inakiliwe kama suala (kipengele kinachojitegemea).
Mifano ifuatayo inaweza kukubaliwa:

1. Kumb. 1/10/2012: Kusomwa na kuidhinishwa kwa kumbukumbu za mkutano uliotangulia

2. Kumb. 2/10/2012: Matumizi mabaya ya dawa

3. Kumb. 10/1: Ripoti ya matukio ya mwezi uliopita n.k.

(e) **Kimalizio**

- Ataje saa za kumalizika kwa mkutano.
- Nafasi ya sahihi na majina ya mwenyekiti na katibu ionyeshwe
- nafasi ya tarehe iandikwe.

II Kaida nyingine zote za usahihishaji wa karatasi hii zitumike.

III Huenda mtahiniwa asiibuke na visa, sababu na namna ya kusuluhisha. Akadiriwe kulingana na namna anavyojieleza, mradi hoja imekamilika.

2. Hii ni insha ambayo inamhitaji mtahiniwa kufafanua/ kujadili mawazo yake au mwelekeo wake kuhusu nafasi ya vijana katika utangamano wa kijamii.

Baadhi ya hoja:

- Vijana ndio wengi hivyo wanaweza kuwafikia raia wengi.
- Vijana wanathaminiana na kuaniminiana, kwa hivyo ni rahisi kuwashawishi wenzao kutangamana.
- Ikiwa vijana watafunzwa maarifa/ mbinu ishi za kukabiliana na matatizo/ changamoto, wataweza kuziwasilisha mbinu hizi kwa wenzao.
- Ni muhimu vijana kuepuka kutumiwa na viongozi kama vyombo vya kuvulia na kupalilia uhasama miongoni mwa raia.
- Kwa kuwa kundi la vijana ndilo lenye nishati zaidi, linaweza kutumia nishati hii katika shughuli zinazoleta utangamano kama vile michezo.
- Vijana wanaweza kujisajili katika vyuo vilivyo katika maeneo mbalimbali nchini ili kutagusana na raia wa makabila tofauti tofauti.
- Vijana wanastahili/ wanaweza kutumia lugha yao (kwa mfano sheng) kama kiungo cha kuwaunganisha na kueneza hisia za kizalendo.
- Vijana wanaosajiliwa katika vikosi vya ulinda usalama wanaweza kueneza siasa/ sera ya kudumisha usalama kwa njia ya amani badala ya vita.
- Vijana wanaweza kukomesha ubaguzi wa kikabila na kinasaba kwa kuhimizana kuchagua viongozi kutoka makabila mbalimbali ili kupalilia mwelekeo wa kitaifa badala ya ule wa kieneo, kikabila au kinasaba.
- Kushiriki katika shughuli za kiusomi kama vile makongamano kunawawezesha vijana kuja pamoja na kujihisi kama raia wenye maazimio sawa, hivyo kuhimiza mshikamano.
- Mshikamano unaweza kudumishwa kupitia ndoa za mseto. Kwa vile vijana wengi si wahafidhina, wengine wao wanaoa na kuolewa na wenzi kutoka makabila tofauti. Uhusiano huu unaunga udugu na kupalilia mshikamano.
- Mradi wa kazi kwa vijana kwa mfano, uliwaleta vijana wa usuli tofauti pamoja.

Powered By: www.manyamfranchise.com

**Tanbihi**

(i) Mtahiniwa anaweza kuchukua mwelekeo wa kuonyesha mambo ambayo vijana wanaweza kufanya ili kuleta mshikamano wa kitaifa.

(ii) Mtahiniwa anaweza pia kuonyesha/ kujadili hatua ambazo vijana wamechukua kuleta mshikamano wa kitaifa.

(iii) Mtahiniwa anaweza pia kuchanganya mielekeo yote miwili, akataja hoja na kuitolea ufafanuzi kwa kuonyesha hatua ambazo vijana tayari wamechukua kuhusiana na suala hili.

3. **Maana ya methali**

Chombo ambacho kimepangiwa kuzama/ ambacho kina kasoro na kinaweza kuzama, hata kikiendeshwa na nahodha wa aina gani kitazama tu.

Jambo la kuharibika hata ukalishughulikia vipi litaharibika tu.

Jambo likiisha kuharibika hata ukajaribu kulirekebisha haitawezekana.

Ruwaza zifuatazo za masimulizi zinaweza kujitokeza.

(i) Mtahiniwa amsawiri msimulizi/ mhusika ambaye anapuuza jambo hadi pale linapoharibika kisha akaanza kulirekebisha. Msimulizi asidiriki kurekebisha jambo hilo. Kisa kibainishe athari mbaya za kutorekebisha jambo mapema.

(ii) Mtahiniwa abainishe hali ambapo licha ya juhudi za mhusika kurekebisha jambo/ kujiimarisha, hafanikiwi. Hapa ni kama jaala inampiga chenga. Mtahiniwa anaweza kuonyesha hiyo ndiyo jaala/ hayo ndiyo majaliwa ya mhusika.

(iii) Mtahiniwa anaweza kuandika kisa kinacholenga kuonyesha umuhimu wa kuyarekebisha mambo kabla ya kuharibika kiasi cha kuzidi uwezo wa mhusika kuyarekebisha.

**Tanbihi**

Masharti ya usahihishaji wa insha za methali yazingatiwe.

4. Mtahiniwa aandike kisa kinachofungamana na mwanzo aliopewa. Hali zifuatazo zinaweza kujitokeza katika kisa:

- Mhusika/ msimulizi amesafiri kwa siku kadha, na ndio anapata fursa ya kupumzika. Anaamshwa na hawezi kuamka.
- Msimulizi anaweza kuwa awali alikuwa katika hali ya hatari, pengine kutekwa nyara na sasa ameokolewa, anajaribu kuamka na hawezi.
- Huenda mhusika/ msimulizi ni muwele hospitalini, anaamshwa na daktari kuhojiwa.
- Msimulizi anaweza kuwa awali alikabiliwa na mgogoro au changamoto iliyompa wasiwasi na kumkosesha usingizi kwa muda.

Kwa vyovyote vile, kisa **lazima** kionyeshe hali ambayo inasababisha **kulimbikiza** kwa usingizi na uchovu na **msukumo** au **kichocheo** cha kuyafumbua macho.

**Tanbihi**

Masharti mengine yote ya utunzaji wa alama katika maswali yote yafuatwe kulingana na kielelezo cha usahihishaji wa insha (mwongozo wa kudumu).

Powered By: www.manyamfranchise.com

## 5.2.2 . Kiswahili Paper 2 (102/2)

1. (a)
- Watoto wananyimwa haki licha ya kuwa katiba inalazimu haki hizi kutimizwa.
- Mojawapo ya haki za kimsingi ni makazi na hali watoto wanalala mitaani.
- Watoto hawapati chakula na hali wanatakiwa kupata lishe bora.
- Wanaotakiwa kulinda haki za watoto ndio wanaozikiuka kwa kuwapiga, n.k.
- Wazazi na jamaa wa karibu wanashiriki katika unyanyasaji wa watoto.

(4 x 1 = 4)

(b)
- Mataifa yasiyo na amani huchangia katika ajira ya watoto. Watoto kutumikishwa vitani.
- Ghasia hupalilia utekaji nyara - watoto wanatekwa kwa lazima na kupelekwa vitani.
- Watoto kuumbuliwa kwa kugeuzwa mababe wa vita.
- Watoto kutengwa na familia zao.
- Dhiki za kimwili na kisaikolojia kwa kuvishwa mavazi mazito na kubebeshwa bunduki nzito.

(3 x 1 = 3)

(c)
- Kubuni sera/mpango wa elimu bila malipo.
- Utekelezaji wa sera hii unaendelea.
- Viongozi baada ya uhuru kubuni mpango / kuandika malengo ya kufikia elimu kwa wote
- Kuna wanaopigania haki ya kuwa kwa elimu bila malipo licha ya matatizo yaliyopo. (Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo).

(3 x 1 = 3)

(d)
- Asilimia ya watoto na watu wazima wasiojua kusoma bado ni kubwa.
- Pengo la kielimu kati ya watoto wa matajiri na maskini bado inaendelea kuwa kubwa.
- Maskini hawamudu kushughulikia mahitaji ya kielimu ya wanao.
- Maskini bado wanalazimika kushughulikia mahitaji ya kielimu ya wanao.
- Miswada inapelekwa bungeni na kupitishwa ila haki hazishughulikiwi kikamilifu.

(2 x 1 = 2)

(e)
(i) Vigogo - walio katika mstari wa mbele / mabingwa.
(ii) Huwa nanga kwao - huwa mazito kwao.
(iii) Kujikuna wajipatapo - kujaribu kujinyanyua kulingana na uwezo wao.

(3 x 1 = 3)

2. (a)
- Uchunguzi unaonyesha Ziwa Viktoria linaangamia polepole.
- Kukauka kwa ziwa (inakisiwa) kutahatarisha maisha ya watu zaidi ya milioni 30 wanaolitengemea kwa chakula na mapato.
- Utafiti wa Taasisi ya Masuala ya Bahari na Uvuvi ulionyesha ziwa linaangamia kwa mita mia tatu kila mwaka.
- Fuo zimekauka upande wa Kenya.
- Shughuli nyingine mbali na uvuvi zinaendelezwa.
- Kupungua kwa rasilimali za samaki kunatishia kuangamiza uvuvi.
- Wavuvi wameingilia biashara nyingine.
- Wengine wanavua katika maji ya mataifa mengine na kuhatarisha usalama wao.
- Gugu-maji limetatiza shughuli za uchukuzi na ukulima.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Kupungua kwa kiwango cha maji kunatishia kukauka kwa ziwa hili.

(yaliyomo - hoja 8 x 1 = 8)
Mtiririko = 1
(alama = 9)

(b)
- Serikali za nchi husika (Afrika Mashariki) ziweke sheria za kudhibiti shughuli za uvuvi.
- Wavuvi washauriwe kufuata kanuni za uvuvi zilizowekwa.
- Serikali za muungano zikomeshe shughuli za kilimo kandokando mwa ziwa na kwenye mito jirani.
- Sheria za kudhibiti matumizi mabaya ya maji ziwekwe.
- Viwanda vinavyotupa taka humu vichunguzwe.
- Juhudi za ustawi wa kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki zizingatie uhifadhi wa Ziwa Viktoria.
- Ziwa likikauka maazimio na malengo ya serikali husika ya kuboresha hali ya maisha yanaangamia

(yaliyomo - hoja 5 x 1 = 5)
Mtiririko = 1
(alama = 6)

3. (a)
- Mzizi wa neno ni sehemu ya neno inayobeba maana ya kimsingi/maana ya kileksia ya neno.
- Sehemu hii haibadiliki hata neno likinyambuliwa / likiambishwa.

mfano: soma, gand-a, sahau-liw-a, ag - a kimbi-li-a, baba, kuku, tak - a
Sehemu zilizopigiwa mstari ndizo mizizi ya maneno husika.

Kueleza - 1, mfano 1 = alama 2

**Tanbihi**

Kuna mizizi huru (kama vile baba, mama, zuri, sahau) na mizizi tegemezi/funge (kama vile som katika soma). Mtahiniwa anaweza kutoa mfano wowote, mradi asadikishe anaelewa dhana ya mzizi.

(b)
- Ata**ku**tengenezea - nafsi ya pili (umoja) / mtendewa /yambwa tendewa (kitondo).
- **ku**le - mahali kusikodhihirika/kiambishi cha ngeli ya mahali. (Ku - Ku)

(alama 1)

(c)
(i) Irabu ya mbele, wastani. /e/ (alama 1)
(ii) Kipasuo ghuna cha kaakaa laini. /g/ (alama 1)

(d) Marashi yaya haya / haya haya ndiyo aliyonunuliwa. (alama 2)
Nomino nyingine: mate, maziwa, mafuta, mazingira n.k.

(e) Maisha ya**li**kuwa ya**me**mwendea vyema. (viambishi li, me) (alama 2)

(f) **Mifano**:
- Mandu huandika vyema lakini Kani huandika vibaya.
- Maskauti walitembea kijeshi ila wanafunzi hawakuvutiwa kamwe.
- Maria atasafiri kesho ilhali Zaina atasafiri mtondo.
- Mwalimu alituita tena lakini Komu hakuitika katu.
- Terry alielekea kushoto na Ndua alibaki katikati.

Powered By: www.manyamfranchise.com

**Tanbihi** (alama 2 / 0)

(i) Hii ni sentensi ambatano.
(ii) Mtahiniwa **lazima** abainishe muundo wa sentensi ambatano.
(iii) Mtahiniwa akikosa sehemu moja atuzwe sufuri (0).
(iv) Aina yoyote ya kielezi inaweza kutumiwa mradi mtahiniwa abainishe mpangilio ufaao wa maneno.
(v) Viunganishi ambatani vitumiwe/asitumie viunganishi vitegemezi.

(g)
- Sentensi changamano huwa na kishazi kimoja huru na kingine kitegemezi.
- Huweza kuwa na vishazi vyote viwili vitegemezi.
- Vishazi huunganishwa kwa viunganishi vitegemezi kama vile, ikiwa, kama, ingawa, iwapo, ki, nge, ngali, ka virejeshi k.v. amba na 'o' rejeshi, n.k.

**Mifano**
- Jamvi lililonunuliwa limechakaa.
- Usahihishaji ukimalizika mapema wanafunzi watapata matokeo.
- Wafanyakazi walijitahidi wakamaliza kazi mapema.
- Ingawa alikuwa maskini aliwaelimisha watoto wake wote.
- Mvua ingalinyesha mapema tungalipata mavuno bora.
- Kama unataka kumwona daktari njoo mapema.

(h) Koga
- uchafu
- fanya maringo
- ondoa uchafu mwilini kwa kutumia maji na sabuni

Konga
- kuzeeka
- kunywa kinywaji/ maji ili kupunguza kiu
- kusanya pamoja/ kukutanisha watu pamoja

**Tanbihi**
Mtahiniwa anaweza kutumia / kuibua maana yoyote mradi kila mojawapo ibainike katika sentensi.

(i) Nomino dhahania - utu, furaha, urembo, wepesi, wema, wivu.

1 x 1 = alama 1

Nomino ya jamii - Kikosi, mkungu, chane, funda, tano, darasa, mfano - darasa la wanafunzi, jeshi, kikosi, umati, halaiki, timu, jamii, familia, hadhira n.k.

1 x 1 = alama 1

(j)
(i) Nywa - nywesha/nywisha
(ii) La - liana
(iii) Vaa - valiwa

(k) **Mifano**
- Julius Kiptoo, mwanawe Kung'u na Justine walikiletea kijiji chao sifa. (Wahusika watatu)
- Julius Kiptoo (mwanawe Kung'u) na Justina walikiletea kijiji chao sifa. (Wahusika

Powered By: www.manyamfranchise.com

wawili) (Julius Kiptoo ni mwana wa Kung'u)
- Julius Kiptoo, mwanawe, Kung'u na Justina walikileta kijiji chao sifa. (Wahusika wanne). (mwanawe - mwana wa Julius Kiptoo au mtu mwingine)
- Julius, Kiptoo (mwanawe Kung'u na Justina)walikiletea kijiji chao sifa. (Wahusika wawili). (Kiptoo ni mwana wa Kung'u na Justina)

**Tanbihi**

(i) Huu ni mfano wa sentensi tata.
(ii) Lazima dhana tatu zijitokeze.
(iii) Mtahiniwa si lazima / hahitajiki kuelezea maana, viakifishi vinatosha.

(l) Naam- kihisishi

Machache - kiwakilishi / kiwakilishi cha idadi ya jumla. (alama 1)

(m)
- Muli alikuwa mwalimu wetu.
- Huyu anaonekana mzima.
- Teddy amekuwa mpole.
- Swali limetuwia gumu.

(alama 2)

(Kitenzi kiwe na kiambishi nafsi au cha ngeli na cha wakati au cha hali)

(n) (i) Shadda ni mkazo unaotiwa katika neno au silabi wakati wa kutamka (alama 1)

(ii) m-te-re-'m-ko (alama 1)

**Tanbihi**
- Mkazo utiwe kwenye silabi ya pili kutoka mwisho wa neno.
- Si lazima atenge silabi.
- Anaweza kupigia mstari

(o) Sahibu - rafiki /mwandani (alama 1)
Kisunzi - kizunguzungu/ kisulisuli (alama 1)

(p) - wa kijinsia - kirai (ki) husishi (neno kuu ni kihusishi 'wa') (alama 1)

- viongozi wenye msimamo (kirai nomino) (neno kuu ni nomino: viongozi) (alama 1)

- thabiti mno - kirai(ki) vumishi
(neno kuu ni kivumishii 'thabiti'

(alama 1)

**Tanbihi**
- Uainishaji ufanywe **kimuundo** wala si **kimajukumu**. Kwa mfano, 'wa kijinsia' ni kirai husishi wala **si** kirai vumishi, japo kinafanya kazi kama kivumishi.

(q) Mama alimwambia Juma kwamba shughuli yao ingemalizika siku ambayo ingefuata. (alama 2/0)

(r) - kiima - watahiniwa hao (alama 1)

- chagizo - kwa makini (alama 1)

Powered By: www.manyamfranchise.com

**Tanbihi**

- **Kiima** ni sehemu ya sentensi ambayo ndiyo habari zake zinatolewa katika kiarifu cha sentensi. Aghalabu huwa kikundi nomino ambacho hutokea kabla ya kitenzi, na kwa kawaida huwa ndicho mtenda katika sentensi.

**Chagizo** ni sehemu ya sentensi ambayo huja baada ya kitenzi au yambwa. Huwa kielezi/ kirai elezi au hata kirai husishi ambacho kinafanya kazi kama kielezi. Ni sehemu ya ziada katika sentensi na huweza kuondolewa bila kuathiri maana ya kimsingi ya sentensi.

(s) Sentensi agizi / amrishi / amri

(inatoa maagizo / maelekezo)

1 x 1 = 1

4. Mazingira

- Mzungumzaji huchota msamiati kutoka mahali anapozungumzia. Kwa mfano, atatumia msamiati wa sokoni akiwa sokoni. Pia kuna lugha ya mahakamani, kwenye mazishi, maabadini n.k.
- Mazingira huathiri kiimbo na hata kidatu. Kwa mfano, mtu akiwa darasani huzungumza kwa kidatu cha chini.

- Mazingira huathiri uteuzi wa msimbo/lugha/lahaja ambayo mtu anatumia. Kwa mfano, mazingira rasmi humtaka mtu kutumia lugha rasmi kama vile Kiingereza na Kiswahili sanifu.

- Mazingira hudhibiti kiwango cha usanifu na urasmi wa lugha. Kwa mfano, mazingira yasiyo rasmi hayahitaji kutumia lugha yenye urasmi au usanifu, mtu anaweza kutumia hata simo/misimu.

- Mazingira hudhibiti mtindo nafsi wa mtu. Kwa mfano, mtu katika mnada au biashara ya rejareja huweza kujirudiarudia ili kuwavutia wateja.

- Ishara anazotumia mtu hudhibitiwa na mazingira. Zipo ishara nyingine za uso au hata miondoko ambayo haikubaliwi/ni mwiko katika baadhi ya tamaduni / mazingira.

- Mtu anayeishi katika mazingira magumu / makali / ya unyanyasaji huelekea kutumia lugha kali au pengine ya matusi, pengine ili kujihami.

4 x 1 = 4

(b) Madhumuni

- Lengo la mawasiliano huathiri jinsi mtu anavyotumia lugha. Kwa mfano, mtu anapoonya hutumia lugha yenye toni kali. Anapotaka kushawishi hutumia lugha ya upole.

- Madhumuni huathiri uteuzi wa msimbo/lahaja/lugha, Kwa mfano, kiongozi anapotaka kuonyesha utangamano na mwanakijiji mwenzake huelekea kutumia lugha ya mama badala ya Kiingereza au hata Kiswahili. Kiongozi huyo huyo huelekea kutumia Kiingereza anapotaka kumtenga mwanakijiji mwenzake.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Madhumuni huathiri kiimbo na shadda. Mtu anapotaka kusisitiza jambo hutia shadda kwenye maneno, au dhana anazotaka kusisitiza. Wakati mwingine hupandisha sauti ili kuwiana na hali ya msisitizo.

2 x 1 = 2

(c) Malezi

- Mtoto aliyelelewa kwa kudhibitiwa huinukia kutoweza/kutomudu kujieleza vyema kwa sababu ya woga aliojazwa.
- Mtoto aliyelelewa katika mazingira ya unyanyasaji hutumia lugha kali ya kujihami.
- Mtoto akilelewa na wazazi wnaozungumza lugha mbili/zaidi ya mbili huweza kujifunza / kutumia lugha zote mbili.
- Mtoto aliyelelewa akihimizwa kujieleza huinukia kuwa na uwezo/ukakamavu wa kujieleza.
- Mtoto asipofunzwa lugha ya mama hushindwa kujieleza kwa lugha hiyo.
- Mtoto hufunzwa kuepuka matumizi ya msamiati/lugha ya aibu/kali, kwa hivyo kutoitumia katika mazungumzo.

4 x 1

**Tanbihi**

Sheria na kaida zote za usahihishaji wa karatasi hii zitumike.

Powered By: www.manyamfranchise.com

### 5.2.3 Kiswahili Paper 3 (102/3)

1. (a) - Hadithi hii inasimuliwa katika nafsi ya kwanza. Usimulizi huu unafanywa na mhusika mtoto/kijana.
- Msimulizi ni mhusika mmojawapo wa hadithini.
- Kuna matumizi ya mofu (ni) na (tu) za nafsi ya kwanza.

kutaja - alama 1
maelezo - alama 2
Jumla - alama 3

(b) Mifano mitatu ya mbinu rejeshi na umuhimu wayo.

(i) Maelezo ya Msimulizi kuhusu usiku ambao babake na watu wengine walizungumza kuhusu mzozo baina ya Wahutu na Watutsi. Babake aliuma kidole. Aidha tunaelezwa kuwa Msimulizi ambaye ni Mhutu alicheza na watoto wengine waliokuwa Watutsi bila kuona tofauti.
Hapa mbinu rejeshi inaonyesha kuwa:
- Watoto hawakuhusika na tofauti za kikabila.
- Watu wazima ndio wenye kuhusika na tofauti za kikabila.
- Mzozo baina ya Wahutu na Watutsi ni jambo lililopangiwa kikamilifu.
- Vita huwatia wasiwasi hata watu wazima.
- Pia mbinu rejeshi inaibua maudhui ya ubaguzi, na uzalendo.

kutaja - alama 1
umuhimu 2 x 1 = 2
Jumla - alama 3

(ii) Msimulizi anakumbuka kuhusu maisha yao shuleni ambapo alisoma na Jesse: UK 119

Umuhimu wake:
- Kuonyesha kuwa msimulizi na Jesse walikuwa na uhusiano mzuri.
- Wote walikuwa hodari katika masomo ya lugha (Kinyarwanda (Jesse) Kifaransa (Msimulizi) (maudhui ya bidii)
- Athari ya ukimbizi - wanaachishwa masomo.

kutaja - alama 1
umuhimu - 1 x 2= 2
Jumla - alama 3

(iii) Msimulizi anawaza kuhusu wema wa Jesse baada ya Jesse kufa. UK 122

Anakumbuka uhusiano wao mwema wakiwa shuleni Rugifare.

Umuhimu wake:
- inaonyesha uhusiano wa kidugu baina yao.
- imani ya Jesse - anamletea msimulizi njugu shuleni.
- kuonyesha mshikamano wa kijamii - wanacheza pamoja.
- kuonyesha dhiki ya kisaikolojia inayosababishwa na ukimbizi.

kutaja - alama 1
umuhimu - 1 x 2= 2
Jumla - alama 3

Powered By: www.manyamfranchise.com

(iv) Msimulizi akiwa safarini kuelekea ng'ambo anakumbuka maneno ya Savalanga, anakumbuka kilio cha uchungu cha mamake na hali iliyomfanya kuwa mkimbizi. (UK 124)

(v) Msimulizi anakumbuka sura ya mama na ndugu zake akiwa Betinga (UK 122).

Umuhimu wake:
- Kuonyesha dhiki ya kisakolojia inayochechewa na vita.
- Kuonyesha maafa yanayosababishwa na vita.

Umuhimu
- inaonyesha uzalendo wa Msimulizi. Anakumbuka kwao, anawazia wasia wa Savalanga.
- inafumbata maudhui ya ujenzi wa jamii mpya kwa kutarajia kutimiza aliyoambiwa na Savalanga.

kutaja - alama 1
umuhimu - alama2
Jumla - alama 3

**Tanbihi**

(i) Mtahiniwa aonyeshe alipo sasa na kusimulia tukio la nyuma.
(ii) Mtahiniwa afafanue kikamilifu mifano yoyote mitatu ili kutuzwa

alama 9.

(c) Vikwazo vinavyoletwa na ukimbizi.

- Kukatizwa kwa elimu - Jesse na Msimulizi wanaacha masomo yao na kukimbilia usalama. (Athari katika sekta ya elimu).
- Kusambaratika kwa familia. Baba ya Msimulizi anaenda vitani.
- Utegemezi. Wakimbizi wanategemea hifadhi/makao katika nchi nyingine. Wakimbizi wanapiga kambi mpakani/kuwa mzigo kwa majirani.
- Ukosefu wa usalama wa chakula. Wanakula matunda-mwitu na wanyama-mwitu, hata mizoga! Uhamishoni chakula ni haba, wanang'angania chakula.
- Wasiwasi/ ukosefu wa utulivu/ ukosefu wa amani. Kila mara wanahofia kushambuliwa. Hofu inamfanya Msimulizi kujikojolea.
- Vifo vya watu ambao wanachangia maendeleo ya nchi- Jesse/ Savalanga, wakimbizi waliouawa njiani.
- Magonjwa/hali duni ya afya, pale kambini/njiani. Jesse na Savalanga wanakufa kwa ugonjwa.
- Dhiki/athari za kisaikolojia. Msimulizi anasikia milio ya bunduki akilini.
- Kutegemea kuelimishwa na jamii nyingine. Msimulizi na wenzake tisa wanapelekwa ng'ambo kusoma.
- Ukosefu wa mshikamano wa kijamii - njiani wanapoulizwa kama wao ni Wahutu au Watutsi wanajawa na woga.
- Hisia za ukiwa - msimulizi anasema walimhurumia Savalanga kwa kupoteza aila yake, hali ambayo inaathiri utulivu wa mtu binafsi.
- Nchi inaachwa bila raia wenye nguvu kuijenga upya. Mzee Savalanga anaonekana kukata tamaa, ndio maana anamuusia msimulizi kurudi nyumbani baada ya vita ili

Powered By: www.manyamfranchise.com

kujenga jamii upya.
- Ukimbizi unaathiri uongozi. Nchi inapoteza vijana kama vile Jesse ambao wangechangia kubadilisha hali ya siasa nchini kwa vile hao hawakutawaliwa na mawazo ya ukabila.
- Makazi duni - njiani na kambini.

(4 x 2 = alama 8)

2. (a) - Ni maneno ya Farashuu kwa Biti Kocho.
- Wamo nyumbani mwa Farashuu Madongoporomoka.
- Biti Kocho amekuja na Maimuna kumchukua Farashuu ukunga.
- Biti Kocho amemhadithia Farashuu jinsi alivyomtoa Maimuna nyumbani na kumzuga kwa kumtajia mapenzi. Ndipo Farashuu akatamka haya.

(4 x 1 = alama 4)

(b) Sitiari - wewe mchawi - kumlinganisha Biti Kocho moja kwa moja na <u>mchawi</u>. (mchawi - bingwa /haini/mjanja)
- Nahau - nakuvika kilemba (nakupongeza/nakustahi).
- Dhihaka / kinaya - Farashuu kumpongeza Biti Kocho kwa uovu.

(2 x 2 = alama 4)

**Tanbihi**

Dondoo limetolewa ukurasa 31.

(c) Uchawi - Ubingwa wa maovu, ulaghai/ujanja/uhaini/ujasiri.

- Biti Kocho anamtoa Maimuna nyumbani kwa ujanja ili kumwonjesha Maimuna mazingira ya uhuru, kusudi Maimuna ashawishike kutoroka.

- Biti Kocho anamchochea Maimuna kuutafuta uhuru. Anamwambia kwamba yeye ni mkubwa si wa kufungwa kama kuku (uk. 27).

- Biti Kocho anakaidi amri ya Maksuudi na kumleta mkunga (Farashuu) kumzalisha Tamima. (Ni bingwa wa ujasiri).

- Anapanga njama kumleta Farashuu ili waweze kulipiza kisasi kwa Maksuudi. (Bingwa wa mikakati ya uovu).

- Yeye na Farashuu wanamtorosha Maimuna na kumtenga na familia yake.

- Ni laghai/mnafiki. Anadai kwamba angalikwenda kumchukua Farashuu lakini anachelea usiku, anataka wa kufuatana naye (Maimuna).

- Anamlaghai Maimuna kuvutiwa na sanamu ya mwanamke na mwanaume ili kumjaza fikira za kutamani mapenzi.

- Ni katili. Anajua aliko Maimuna lakini hamwambii Tamima. Hata kengele inapobonyezwa anajidai kwamba labda ni Maimuna na hali anajua siye.

- Anathubutu kumkabili Maksuudi na kumwambia kwamba kumpiga Tamima hakutabadilisha lolote. (Ujasiri).

- Anamshutumu Maksuudi kwa ukatili wake. Anamlaumu Maksuudi kwa kumtawisha Maimuna. Anathubutu kumwita Maksuudi mjinga. (uk 51) anapodai kuwa wanawake

Powered By: www.manyamfranchise.com

hawajui siasa.

- Anapoona Tamima ataumizwa zaidi anasimama mbele ya Tamima na kumkinga. / Ana tambo ambalo linamfanya Maksuudi kunywea. Maksuudi anaona kwamba ingawa Biti Kocho ni mwanamke, hana tani yake (52).

- Anamwombea Tamima talaka na kusambaratisha ndoa yake.

- Anahakikisha ya kwamba amemchungachunga Tamima wanapoondoka kwa Maksuudi, anamshauri aende kwao shamba na hata kuhakikisha amepata usafiri (torinkaa) kuelekea huko.
- Ni fisadi. Anamwomba Farashuu shilingi mia mbili kumpa karani wa viwanja hongo amfanyie mpango kupata kiwanja fulani.

- Ni mwenye mbinu za ushawishi/ana uwezo mkuu wa kushawishi. Anatoa maelezo ya kushawishi (wakiwa pale nyumbani kwa Tamima), (wakiwa njiani na Maimuna) kuhusu umuhimu wa kumleta mkunga nyumbani na baadaye utamu wa mapenzi.

( Hoja 6 x 2 = alama 12)

3. – Wanawake wanachangia katika kusambaratika kwa asasi ya familia. Kazija, Farashuu, Biti Kocho wanasambaratisha familia ya Maksuudi.

– Wanawake wanamnyima Maimuna na kile kitoto kichanga cha Tamina haki ya malezi. Farashuu anashirikiana na Biti Kocho kumtorosha Maimuna. Biti Kocho anachochea kutalikiwa kwa Tamima ambaye anakiacha kitoto kwa Maksuudi, kitoto kinakufa.

– Wanawake ni vyombo vya uzinifu ambavyo vinasababisha mafarakano katika ndoa. Kuhusiana kwa Kazija na Maksuudi kunamnyima Tamima uwepo/ushirika wa Maksuudi; Tamima anapopata uchungu wa uzazi mumewe hayupo. Wanawake pale Bobea, mfano Maimuna, wanampigania Shoka ambaye hamjali mkewe Selume. Wanawake wanamwingiza Maimuna katika ukahaba. Farashuu anapomtorosha Maimuna anampeleka kwa Mama Jeni (danguroni) ambako anaingilia ukahaba.

– Mama Jeni anawatumia wasichama kama vitega uchumi. Anapanga njama ya kumkutanisha Maimuna na James kwa malipo ya shilingi ishirini. Dora anaishi kwa Mama Jeni akifanya ukahaba, anasema ana deni la kulipa kwa Mama Jeni.

– Farashuu anamnyima Maimuna nafasi ya kukulia katika mazingira ya nyumbani kwao (Liwazoni) kwa kumtorosha.

– Mama Dora anamnyima Dora haki ya malezi kwa kumuuza kwa Mama Jeni.

– Biti Sururu anamwingiza Maimuna katika uuzaji wa pombe pale 'kil mi kwiki'.

– Biti Sururu anamfanya Maimuna kutumia pombe vibaya kwa kumwingiza katika mazingira kunakouzwa pombe. Maimuna analewa hadi kikohozi chake kinachanganya harufu ya damu.

– Mwanasururu anajaribu kumshurutisha Kabi kutenda lisilofaa. Kabi anatoroka na kuishia kugongwa na gari na kupoteza mguu wake.

– Farashuu anamdhalilisha Maimuna mbele ya Kabi kwa kumwita mhuni.

Powered By: www.manyamfranchise.com

– Wanawake pale pa Mama Jeni wanamsingizia Maimuna wizi na hali siye aliyeiba. Mama Jeni anamfukuza bila hata ithibati kuwa ndiye aliyemwibia.

– Maimuna anapotambua uhuni wa Farashuu na Biti Kocho, na Mama Jeni, badala ya kurudi nyumbani anasema heri aendelee kuishi katika shimo hili badala ya kurudi kwa Tamima. Anamkosesha mama yake mapenzi ya mama na binti.

– Maimuna anamuumbua baba yake pale Rumbalola na kwa Biti Sururu. Anamkana babake na hata kumsababishia kifo kutokana na kihoro cha kukataliwa.

– Kazija anampigisha Mussa kwa babake kwa kuwakutanisha na hata kujaribu kumchochea Maksuudi kumpiga Mussa.

– Udhaifu wa Tamima unamfanya asiweze hata kumtetea Maimuna anaponyimwa elimu rasmi. Anafundishiwa ndani.

– Maimuna anamwibia Ashuru kwa hila na kukiuka haki ya kuheshimu milki ya watu.

– Farashuu anawatumikisha wasichana kwa saa nyingi.

– Kijakazi anamtukana na kumuumbua Maimuna hadharani.

(Hoja 10 x 2 = alama 20)

4. (a) (i) – Maneno ya Zigu
- Anamwambia Kaloo
- Wamo katika kisima cha Mkomani/Bonde la Ilangi ambamo Kaloo amemfuata Zigu.
- Kaloo anamwomba Zigu amshukuru Bokono kwa kuamrisha mtoto wa Kaloo kupewa kazi.
- Ndipo Zigu anamwambia Kaloo haya. (4 x 1 = alama 4)

(ii) Mwongo/mdanganyifu/mnafiki.
Anasema kwamba Bokono anapenda watoto sana na hali anajua kwamba Bokono ameidhinisha kuchukuliwa kwa uwanja wa kuchezea watoto.
(kutaja) - 1 (kueleza - 1) (alama 2)

(iii) Vichocheo
- kutaka kutambuliwa
- ulimbukeni/usungo
- kutaka kujitambulisha na wakubwa
- woga
- tamaa ya mali/mamlaka/ubinafsi
- kujikomba kwa wakubwa/kutaka kuonekana mwema/mjuzi na Kaloo.
- Udikteta wa Bokono unamfanya kuwa mnafiki ili kufaidika kwaye / asiadhibiwe.
- Hali ya uhitaji Butangi inamfanya yeye na wenzake kutaka kuvutia kwao tu.

(4 x 1 = alama 4)

Powered By: www.manyamfranchise.com

**Tanbihi**
Dondoo limetolewa uk 89

(b) - Baadhi wanaendeleza uongozi dhalimu badala ya kuupinga. Kaloo anakwenda uwanjani kuandalia mkutano wa Bokono badala ya kuususia. Gege anafika uwanjani kupiga ala. Washauri wanamsifu Bokono kiongo badala ya kumkosoa.

- Ubinafsi na tamaa unawafanya wengine kutumiwa kama vikaragosi. Gege anamuua Mwelusi ili kufanikisha uongozi wa Bokono.

- Askari II, III na makachero, kwa kujiona kuwa katika kundi sawa na Bokono, wanafuata kanuni kandamizi za gereza na kuishia kuwanyanyasa wanyonge wenzao. Askari II, III wanamnyima Mwelusi chakula, Mweke na Talui wanampiga Mwelusi. Askari II na kikosi chake wanamuua mtuhumiwa na kumzika msituni.

- Wanawake wanaridhia kutumiwa kama vyombo vya burudani. Kaloo anashangaa ikiwa hawatamkatikia Mtemi watamkatikia nani?

- Wanyonge wanamwimbia Mtemi nyimbo za kumsifu kiongo badala ya kumkosoa. Wanasema wamshukuru Mungu kwa zawadi adimu (Bokono) na hali anawadhulumu. Wengine wanakwenda Ikuluni kumhakikishia Mtemi uzalendo wao. (mf Kijiji cha Mipashoni Uk. 102)

- Baadhi wanaombea utawala wa Bokono udumu. Askari II anaomba Mungu ampe Bokono maisha marefu ili azidi kumhifadhi na huku anazidi kuwanyanyasa wanyonge.

- Wengine wanataka kurithi/ kuendeleza mfumo kandamizi. Askari I anataka kumwangamiza Bokono kwa shoka lakini Atega anamkataza.

- Tanya anapuuza uhasama kati ya Gege na Mwelusi, anamwelekeza Gege kwa Mwelusi, Gege anaishia kumuua Mwelusi/Ingawa Gege ni mnyonge kama Mwelusi anakubali kutumiwa kama chombo cha kumwangamiza Mwelusi.

- Ujasiri wa Mwelusi, badala ya kumfaa unamsababishia kupigwa na Mweke na Talui. Mwelusi anakataa kusema anampenda Bokono, jambo ambalo linawafanya Mweke na Talui kumpiga sana.

- Mwelusi anakataa ushauri wa mamake kuwa aondoke Butangi; anaishia kuuawa kwa amri ya Bokono. (Anapuuza uhasama baina yake na Gege).

– Raia wanaruhusu viongozi wanarithi mfumo kandamizi na kuuendeleza. Uongozi dhalimu umekuwepo tangu enzi za Mtemi Mulima na wengine kama Bokono hawawazii kuubadilisha.

(10 x 1 = alama 10)

5. Ufaafu wa anwani

(i) Mtahiniwa abainishe maana ya juu - Kifo cha Mwelusi kinatokea katika Kisima cha Mkomani.

(ii) Maana ya Kiistiari

Powered By: www.manyamfranchise.com

Kifo ni sitiari ya mateso/maangamizi/kutofikia malengo au maazimio/ uozo/ tandabelua/ machafuko.
Kisima ni sitiari ya nchi/ taifa/ chemchemi ya uhai / hifadhi ya raia.
- Mtahiniwa aonyeshe kinyume cha mambo.
Badala ya Kisima/ nchi kuwa chemchemi ya uhai/ fanaka, viongozi wanakuwa watesi wa raia/ wanawaangamiza raia. Hoja zifuatazo zinaweza kuzingatiwa:

- Viongozi wanawanyima raia uhuru wa kuchota maji kisimani - wanaruhusiwa kuchota siku tatu tu kwa wiki.
- Viongozi kuwapiga raia kinyama - Mwelusi anapigawa na Mweke na Talui gerezani. Mtuhumiwa anapigwa na Askari II na kikosi chake msituni. Andua na mtoto wa Chendeke wanapigwa
- Wapigania haki kufungwa gerezani - Mwelusi anafungwa kwa madai kuwa ni kiongozi wa Kabakaba/anawachochea raia, yeye na wenzake wa kikundi cha Nuru ya Butangi.
- Sera mbovu za uongozi - kutumia propaganda. Batu anamwambia Mwelusi awatangazie raia kuwa uchochezi unaletwa na majirani na hali sivyo.
- Unyakuzi wa mali ya umma - Mgawa ardhi anachukua uwanja wa kuchezea watoto na kumpa Askari Mkuu. Bokono ananyakua Bonde la Ilangi.
- Viongozi **wanaharibu mazingira** wanalima na kulisha wapendapo, hivyo kuumomonyoa udongo.

- Viongozi kuwatelekeza raia katika njaa. Mwelusi anasema Butangi imejaa njaa.

- Viongozi kutowahakikishia raia **usalama** . Batu anawalipa wahuni kuwashambulia Balusi na kusababisha uharibifu wa mali.

- Viongozi **kuwatenga** raia badala ya **kuwaunganisha**. Batu anapowalipa wahuni kuwashambulia Balusi Batuitui wanasingiziwa ili kuzua chuki baina yao na kuupujua mshikamano wao.

- Maandamano ya raia kupinga uongozi dhalimu. Balusi wanaandamana. Hili lasababisha taharuki kwa uongozi / uongozi unalipiza kwa kushambulia.

- Washauri wa Bokono wanaudhoofisha uongozi wake. Badala ya kumshauri aache uongozi mbaya wanamsifu kiongo. Wanasema yeye ni mwenye busara.

- Gege anausaliti udugu wake na Mwelusi, anamuua Mwelusi.

- Maandamano ya mwisho ya raia wakiongozwa na Atega yanamng'oa Bokono mamlakani, hivyo kuuangamiza (kuuua) uongozi wake. (Mapinduzi)

- Badala ya Bokono kupevuka kimawazo anarudi nyuma. Nyalwe anamwigiza Bokono akirudi nyuma kutoka utuuzima, makamo, ujana, utoto hadi anapokuwa kijusi kwenye mji wa mama yake.

- Uozo - Bokono anadhaniwa kuwa na hawara aliyepigwa na Nyalwe. Zigu anamwambia Kaloo kuwa jicho la Mtemi limemwona. Askari III anajaribu kumshika Andua kifuani.

- Ufisadi - ugavi usiofaa wa mali ya umma. Mgawa ardhi kumpa Askari mkuu uwanja wa kuchezea watoto. Bokono anaidhinisha haya. Bokono anampa mtoto wa Kaloo kazi kwa sababu Kaloo ni kikaragosi wa Bokano.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Unafiki wa viongozi. Batu anajidai kuwa rafiki wa Tanya ili Tanya amwelekeze aliko Mwelusi. Batu anajidai anamjali Mwelusi pale gerezani. Mweke na Talui kujidai wanamstahi Gege, Mweke anamwahidi Gege kuozwa Alida, huku akijua si kweli.

- Mauaji - Mtuhumiwa kuuawa na kuzikwa msituni, Mwelusi kuuawa na Gege.

- Chuki ya ndugu - Gege anamwonea Mwelusi wivu. Badala ya kwenda kumtazama gerezani anatengeneza ala.

- Dhiki ya kisaikolojia - Wasiwasi unamfanya Tanya kuwa na jinamizi.
- Ukosefu wa umoja miongoni mwa vijana. Badala ya Gege kujiunga na akina Mwelusi, anawapinga na kusema wanamchukia Bokono.

- Sheria/baraza la hukumu na vyombo vingine vya dola kama vile polisi wanalinda maslahi ya Bokono badala ya umma.

- Uongozi kutolipia huduma. Mbutwe halipwi kwa kutengeneza viti vya kutumiwa na mkutano wa Bokono.

- Asasi za kurekebishia sheria zinapunza haki za wafungwa Mwelusi ananyimwa chakula na fursa ya kutembelewa na jamaa.

(10 x 2 = alama 20)

**Kumbuka**: Lazima hoja mojawapo iwe ile maana ya kijujujuu.

6. (a) - Ni safari ya kupigania uhuru/ safari ya kutafuta haki/ safari au harakati za kujiendeleza kiuchumi. Anasema walishikana kwenye safari ya haki, walisita kwenye mlima wa haki. Anataja kuteremsha miliki.

Kutaja - alama 1
Kueleza - alama 1

(b) Maelezo ya (maana ya) kinaya yawepo.

- Kinyume cha matarajio, (viongozi) wachache waliofika kileleni walijawa na uchoyo, wakaamua kujinufaisha. (alama 1)

- Walijitengenezea makazi ya raha, wakajinyakulia vyeo wakakaa kufurahika/huku wakiwasahau waliowakweza mamlakani.

- Wakawa ndio pekee waliofaidi matunda ya uhuru ambayo yalikuwa yamepiganiwa na wote.

- Viongozi wamefika hadi kuwadhuru raia waliowapa hivyo vyeo - wanawatemea mate.

- Raia kupigania uhuru na baadaye kutofaidika kwao.

- Kutofikia maazimio ya kiuchumi. Hawapati milki waliopigania

- Safari ya haki na hali ubaguzi unajitokeza.

(5 x 1 = alama 5)
(- kueleza kinaya/ kujitokeza kwa kinaya - alama 1)
**Jumla - 6**

Powered By: www.manyamfranchise.com

(c) (i) Msuko - Mshororo wa mwisho una mizani chache kuliko mingine/ umefupishawa.

(ii) Ukara - Vina vya kati/ ndani vinabadilikabadilika. Vya nje/ mwisho vinatiririka.
(2 x 2 = alama 4)

(Kutaja - 1, Kueleza - 1)

(d) Mfano:
Wawakilishi/viongozi walijikuta katika hali nzuri sana za maisha na tamaa ya kujinufaisha ikazidi. Walishiriki starehe za kila aina. Katika hali hii walisahau wananchi/ raia waliowakweza katika nafasi hizo (waliowapa nafasi hizo) za uongozi, na ambao ndio waliokuwa na nyenzo za kuwafanya kufikia hali hii yao (viongozi) ya sasa.
(alama 4)

(e)
- Inkisari tukawa'chia - kutosheleza idadi ya mizani.
- Kufinyanga sarufi/kuboronga sarufi/kubanaanga lugha/miundo ngeu ya kisintaksia.
- Kialeni wadiriki - wadiriki kileleni - kuleta urari wa vina.
- Tabdila - shaki - badala ya shake - kuleta urari wa vina.
- Lugha chakavu/msamiati kikale.
- Kialeni - Kileleni
- Kulipa shairi mapigo ya kimuziki
- Kulipa shairi upeke wa kiutanza.

(kutaja - alama 1, maelezo; alama 1)
(2 x 2 = alama 4)

7. (a) (i) Maana ya Kijujuu.

- Ni chai ya jioni.
- Inanywewa na mume na mke huku wakiwatazama watoto wakicheza bembea.
- Chai inakaribia kumalizika.
- Mzungumzaji anamtaka mwenzake wahakikishe wameviacha vikombe vyao vikiwa safi.

(3 x 1 = alama 3)

(ii) Maana ya kitamathali.

- Shairi ni sitiari ya maisha yao ambayo yanakaribia kumalizika. Wameanza kuzeeka.
- Bembea - Sitiari ya maisha yao ya ndoa/ safari yao ya maisha/ chai ya jioni (Ushirika/uwepo wao katika siku za mwisho au maisha yanavyokaribia kuisha.
- Waliyopitia katika maisha yao ya ndoa - chamgamoto na furaha (kulikuwa na wakati lipokudaka ulipokaribia kuanguka).
- Maazimio ambayo hawakufikia - (sasa tukisubiri ndoto tusizoweza kuzitekeleza tena.
- Mume/ mke anamtaka wamalizie siku zilizobaki vyema.
- Anamkumbusha siku walipokutana mara ya kwanza wakijaribu kujenga urafiki/ kuchumbiana.

(3 x 1 = alama 3)



Powered By: www.manyamfranchise.com

(b) (i) Usimulizi.

- Nafsineni inasimulia wakati walipokuwa wakicheza bembea/jinsi walivyofurahia maisha pamoja kwa matumaini.
- Anasimulia siku walipokutana.

Mfano - 1 x 2 (alama 2)

(ii) Usambamba.

Huu ni urudiaji wa muundo sawa/ huo huo wa mshororo/sentensi.

Mfano:
- kulikuwa na wakati ulinisukuma juu.
- kulikuwa na wakati nilikudaka.

Mifano - 2 x 1 (alama 2)

(iii) Taswira
- Pana picha ya watu wanaokunywa chai na watoto wanaocheza bembea.

- Picha ya wenzi wa ndoa wenye furaha/wenye ushirikiano/wanaoongozana jikoni kupika.

- Picha ya watu wakitafuta tawi la kufungia bembea, na mbwa akiwasubiri.

- Picha ya nafsineni/mshirika katika ndoa anayemwambia mwenzake (kwa masikitiko) maisha yao karibu yanafikia kikomo.

Mifano - 2 x 1 (alama 2)

(c) Nafsineni - ni mzuugumzaji au msimulizi katika kazi ya kifasihi. Nafsineni katika shairi hili ni mwenzi katika ndoa (mume au mke). Anasimulia walivyokutana, anataja watoto wao.

(kutaja - 1, Kueleza - 1)
(alama 2)

(d) - Toni ya mchanganyiko wa furaha matumaini na masikitiko/huzuni

(alama 1)

Mifano:

(i) Mzungumzaji anasimulia maisha yao ya furaha; kucheza bembea, kupika pamoja...

(ii) Hata hivyo anaonyesha haya karibu yatafikia kikomo, anasema wamalizie chai yao ya jioni.

(iii) Kuna maazimio yasiyofikiwa - anasema wanasubiri ndoto wasizoweza kuzitekeleza tena.

(iv) Anakumbuka kwa furaha na masikitiko siku yao ya kwanza kukutana.

(v) Ana matumaini ya kumalizia machicha (masalio) ya chai yao.

(3 x 1 = alama 3)

Powered By: www.manyamfranchise.com

(e) - Kutenda mema

- Kurekebisha yaliyo kombo katika maisha/ uhusiano wao na wanajamii wenzao uwe wa kuridhisha.

- Kukamilisha/ kutimiza waliyoazimia kutimiza. (Hoja 1 x 2 = alama 2)

8. (a) - Nyimbo huhifadhi historia ya jamii, kwa mfano, nyimbo za sifa, nyimbo za siasa, nyimbo za vita.

- Huhifadhi na kupitisha utamaduni k.v. mbolezi hubeba utamaduni wa jamii kuhusu kifo, mazishi.

- Kuliwaza - k.v. mbolezi.

- Kuonyesha ustadi/ ubora wa jamii - wimbo bora/ mwema huonyesha ubora wa msanii.

- Kuhamasisha, kwa mfano nyimbo za kisiasa huhamasisha kupinga udhalimu.

- Kuelimisha - nyimbo za kazi (hodiya) hufunza maarifa ya kazi kama vile ukulima na usasi.

- Hukuza utangamano - Nyimbo za kazi, watu wanapoimba pamoja hujihisi kuwa kundi moja.

- Ni njia ya kutakasa hisia. Nyimbo za mapenzi na mbolezi hutumiwa kutoa hisia za moyoni.

- Huadilisha - Nyimbo hufumbata maadili ya kijamii na kidini. Kwa mfano nyimbo za kidini, bembelezi na hata mbolezi.

- Kukashifu tabia hasi - K.v. nyimbo za jandoni (nyiso) kukashifu woga.

- Kusifu tabia chang - K,v, sito

- Hukuza uzalendo - Wimbo wa taifa, nyimbo za kisiasa/huhimiza raia kujitoa mhanga kwa nchi.

- Kuimarisha ubunifu - Kadiri mtu anavyoimba ndivyo anavyonoa stadi za utunzi na uimbaji.

- Ni nyenzo ya burudani. Takriban aina zote za nyimbo hulenga kuburudisha tumbuizo.

- Hurithisha sanaa yenyewe ya uimbaji na utunzi wa nyimbo kwa vizazi kwa kuziimba kutoka kizazi hadi kingine.

- Hutumiwa katika vipera vingine kama vile ngano kuhuisha hadhira.

(5 x 2 = alama 10)

**Tanbihi**

Mtahiniwa <u>sharti</u> atoe mifano ya aina za nyimbo zinazotekeleza majukumu aliyotaja.

(g) Illi kufanikisha uwasilishaji wa wimbo, mwimbaji anahitaji:

- kuwa na sauti ya kuvutia ili kuvuta makini ya hadhira/kuiwezesha hadhira kupata ujumbe, kuihuisha kupata ujumbe.
- kuihusisha hadhira, kwa mfano, kupitia kwa kupiga makofi ili kukinga dhidi ya ukinaifu.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- kutumia udramatishaji/ uigizaji ili kusisitiza ujumbe/ kuufanya wimbo kuvutia/ kuifanya hadhira kukumbuka.
- kuelewa hadhira ili kuubuni wimbo upya/ kutumia mtindo ufaao kuuwasilisha.
- kuuelewa utamaduni wa hadhira ili kukinga dhidi ya kutumia maneno/ishara zinazokinzana na utamaduni huo.
- Kutumia viziada lugha kama vile ishara za uso na kidatu kusisitiza ujumbe.
- Awe mkakamavu ili awasilishe wimbo bila kuogopa hata kama unashirikisha masuala ambayo ni mwiko/nyeti.
- Aelewe lugha ya hadhira ili aweze kuitumia kufanikisha uimbaji wake.
- Awe mbunifu wa kuweza kuubuni wimbo upya kulingana na hadhira. Wimbo wa watoto uhusishe nyenzo kama vile mchezo wa sauti na maneno.
- Awe mfaraguzi ili kuuimba wimbo kwa mahadhi tofauti tofauti ili adumishe mvuto.
- Ahusishe masuala ibuka/ masuala yanayoiathiri jamii wakati huo ili kupitisha maadili yafaayo.
- Awe na kumbukumbu nzuri ili aweze kuzirithisha nyimbo kama alivyoimbiwa (kifani na kimandhui) bila kubadilisha sana.
- Avae maleba yanayoafikiana na wimbo anaowasilisha ili kurahisisha uelewa wa ujumbe.
- Abadilishe toni kulingana na ujumbe anaopitisha ili kuibua taathira ifaayo kwa msikilizaji.
- Kutumia ala kwa njia mwafaka ili kukuza mvuto wa utungo wake.

**Tanbihi**

Mtahiniwa <u>lazima</u> atoe ufafanuzi toshelevu/unaoridhisha ili kutuzwa alama <u>2</u> kwa hoja.

(5 x 2 = alama 10)

Powered By: www.manyamfranchise.com

- kutumia udramatishaji/ uigizaji ili kusisitiza ujumbe/ kuufanya wimbo kuvutia/ kuifanya hadhira kukumbuka.
- kuelewa hadhira ili kuubuni wimbo upya/ kutumia mtindo ufaao kuuwasilisha.
- kuuelewa utamaduni wa hadhira ili kukinga dhidi ya kutumia maneno/ishara zinazokinzana na utamaduni huo.
- Kutumia viziada lugha kama vile ishara za uso na kidatu kusisitiza ujumbe.
- Awe mkakamavu ili awasilishe wimbo bila kuogopa hata kama unashirikisha masuala ambayo ni mwiko/nyeti.
- Aelewe lugha ya hadhira ili aweze kuitumia kufanikisha uimbaji wake.
- Awe mbunifu wa kuweza kuubuni wimbo upya kulingana na hadhira. Wimbo wa watoto uhusishe nyenzo kama vile mchezo wa sauti na maneno.
- Awe mfaraguzi ili kuuimba wimbo kwa mahadhi tofauti tofauti ili adumishe mvuto.
- Ahusishe masuala ibuka/ masuala yanayoiathiri jamii wakati huo ili kupitisha maadili yafaayo.
- Awe na kumbukumbu nzuri ili aweze kuzirithisha nyimbo kama alivyoimbiwa (kifani na kimandhui) bila kubadilisha sana.
- Avae maleba yanayoafikiana na wimbo anaowasilisha ili kurahisisha uelewa wa ujumbe.
- Abadilishe toni kulingana na ujumbe anaopitisha ili kuibua taathira ifaayo kwa msikilizaji.
- Kutumia ala kwa njia mwafaka ili kukuza mvuto wa utungo wake.

**Tanbihi**

Mtahiniwa lazima atoe ufafanuzi toshelevu/unaoridhisha ili kutuzwa alama 2 kwa hoja.

(5 x 2 = alama 10)

Powered By: www.manyamfranchise.com